

**REPUBLIC OF KENYA**  
**COUNTY ASSEMBLY OF LAIKIPIA**  
**THE HANSARD**

**Wednesday, 7<sup>th</sup> December, 2022**

*The House met at the Assembly Chambers at 2.30 p.m.*

*[The Speaker (Hon. Lantano Nabaala) in the Chair]*

**PRAYERS**

**MOTION**

REVIEW OF WATER TARIFFS

**Hon. Stephen Ndiritu:** Asante, Mheshimiwa Spika. Nilikuwa na mjadala wa development of small and micro-enterprises policy ambayo ilikuwa ifanyike asubuhi. Nilikuwa pia nimepatiwa nafasi na Mheshimiwa Gathoni ili niweze kuendeleza mjadala mwingine lakini nikiangalia kwa hii tarakilishi, haina huo mjadala. Naomba nipatiwe ili niweze kuendelea. Hon. Speaker, I beg to move the following motion;

THAT, AWARE THAT Article 43(1) (d) of the Constitution of Kenya stipulates that, every person have the right to clean and safe water in adequate quantities;

FURTHER AWARE THAT Section 72(1&2) of the Water Act, 2016 provides that, the powers and functions of the Regulatory Board shall be to determine and prescribe national standards for the provision of water services and asset development for water services providers, evaluate and recommend water and sewerage tariffs to the county water services providers and approve the imposition of such tariffs in line with consumer protection standards;

NOTING THAT pursuant to section 38(1) of the Water (Service Regulatory) Rules, 2012, the Regulatory Board may, on its own motion or pursuant to a complaint investigate any tariffs charged by a licensee;

CONCERNED THAT the Water service providers in the County namely Nanyuki and Nyahururu Water and Services Companies charged exorbitant tariffs during the last review;

OBSERVING THAT Water tariff reviews are usually done every three years;

COGNIZANT THAT, water and sewerage services are devolved function;

This House URGES the County Government to partner with the Water Services and Regulatory Board with a view to reviewing the tariffs downwards.

Asante, Bwana Spika. Huu ni mswada ambao unalenga kusaidia mwananchi wa Laikipia sanasana Nanyuki na Nyahururu. Kampuni ya NAWASCO na NYAHUWASCO imekuwa ikilipisha mwananchi wa kawaida pesa ambayo haiambatani na sheria. Bwana Spika, naomba Waheshimiwa waweze kupitia huu mswada na kuweza kuangalia vile sheria inasema na vile

tutafanya ili kusukuma serikali mpaka iweze kuhakikisha ya kwamba maji imelipishwa kwa bei ambayo inafaa.

Bwana Spika, wakati nilikuja Nanyuki mwaka wa tisini na tisa, nilikuta bili ya maji ikiwa haijafika mia moja. Kwa sasa bili ya maji hasa kwa wale ambao wako nyumbani imeenda juu zaidi ya mia tano na kuendelea. Hii inaonyesha kwamba mwananchi ambaye anaishi Thingithu, Majengo, Sweetwaters, Nturukuma na Likii amekuwa akilipishwa pesa kwa njia ambayo haifai.

Kwa hivyo Bwana Spika, NAWASCO hawafai kuchukua sheria mkononi ila wanafaa kufanya ushiriki wa umma ili waweze kuuliza wananchi vile wanataka kwa sababu hata kama ni biashara tunafanya, hata mimi nikiwa soko huwa naonega na wateja ili tusikizane. Nikisikia nitaweza bei yake, nitamuuzia hiyo bidhaa. Nikisikia bei yake imerudi chini, nitaamua kuuzia mwingine ama nibaki na mali yangu.

Kwa NAWASCO kwa sababu ndio nawaelewa zaidi, waliweza kuchukua mali yao, wakapeleka soko, wakaweka bei na kisha kukuambia uchukue ama usichukue utapata kwa nguvu. Hilo ndilo limekuwa likifanyika hapa Nanyuki. Wananchi wanalia katika kila sehemu. Ukishindwa kulipa pesa ambayo wameweka shilingi mia tano au mia mbili na hamsini, wanakupiga faini ya elfu moja juu ya hiyo bili.

Bwana Spika, sisi kama wakilishi wa wananchi tumesikia kilio chao na ndio maana tunaleta huu mswada wa kuweza kuomba Bunge hili, pamoja na Serikali ya Utawala na NAWASCO, ili wateremshe bei kulingana na vile maisha iko. Wakati huu Bwana Spika, tunaonega kuhusu *bottom-up*. Mimi hupenda kuongea kuhusu *bottom-up* kwa sababu nilichaguliwa na chama cha UDA. Wakati tulikuwa tunafanya kampeni tulisema tutateremsha bei ya unga na vitu vyote.

Ni vile tu hatujafikia kuteremsha bei ya mahari kwa sababu inafaa kuteremsha kila kitu. Sisi ni watu wa *bottom-up*. Bwana Spika, sisi tunaanza na maji ili turudi kwa hizo zingine. Ndio maana naomba Wabunge, tuungane pamoja tukatae mwananchi kulipishwa faini ya elfu moja. Kama mtu ameshindwa kulipa shilingi mia mbili, hakuna sheria imesema umlipishe mara tano zaidi. Hiyo ni kukosa ubinadamu na kuona kwamba sababu nyinyi ndio mko na maji mnaweza kufanya vile mnataka.

Bwana Spika, kama tutakubaliana leo na huu mswada upite, jioni kama mkurugenzi wa NAWASCO na NYAHUWASCO hawatateremsha bei ya maji, itabidi tuwatoe ofisi. Nafikiri tumepatiwa jukumu na wananchi kuja hapa kuwatetea. Tumepatiwa mamlaka na sheria kwa niaba ya wananchi ili tuweze kuwatetea. Mwananchi ambaye yuko Baraka, Likii na sehemu zingine kwa sababu hawezi kufika hapa ndio maana leo nimevaa suti na tai nije hapa kumtetea na nihakikishe ya kwamba hiyo bili imerudi chini.

Nitakuwa na jukumu ya kufuatilia na kuhakikisha mswada ukipita, maji itateremka. Kwa sababu hawa wakurugenzi wamekuwa na vichwa ngumu saa zingine, itabidi sisi sote tuungane. Wale ambao tunawakilisha Nyahururu, Nanyuki na wadi ambazo zinazungukwa na NAWASCO na NYAHUWASCO, tutakuwa na jambo la kuingia katika hizo ofisi ili tuwaambie tumepitisha wateremshe hiyo maji.

Kwa hivyo Bwana Spika, nafikiri huu mswada umekuwa kwa wakati ambao unafaa. Manifesto ya Gavana inaambatana na huu mswada. Nimesikia Gavana mwenyewe akiongea mara

tatu akisema tunataka maji iteremke. Pengine naweza kukosa kitu cha kujishikilia ili kuteremsha hiyo maji kwa sababu ni lazima utumie sheria ili uweze kufanya kazi hasa kwa hizo kampuni.

Kwa hivyo, tutampatia sheria ambayo tutapitisha hapa. Nikiangalia Waheshimiwa, naona wanaona umuhimu wa kupunguza maji. Bwana Spika, kampuni ya NAWASCO na NYAHUWASCO iko na sehemu ambayo utapata wameweka bomba na mita na maji haifiki. Vilevile, ikifika mwisho wa mwezi wanaleta bili mpaka mwananchi anashindwa ni upepo umekunywa ama ni nini.

Sisi tukiwa Waheshimiwa, kazi yetu ni kuhakikisha ya kwamba tumelinda na tumetetea wananchi kulingana na sheria ambayo iliwekwa. Maji ambayo NAWASCO wanachukua kwa ulaji wamepewa hiyo maji kupitia *Water Services Regulatory Board*. Nafikiria wamepewa sheria ambayo haiwaruhusu kulipisha mwananchi vile wanataka. Bwana Spika, nikisoma hii sheria ninaona kama wamekiuka hiyo sheria.

Mwananchi hajui kama sheria imekiukwa. Sisi ndio tumejua sheria imekiukwa. Bwana Spika, saa zingine itabidi tusimame kidete tutetee mwananchi na tutamtetea leo na kama sio leo, ni sasa hivi. Huu ndio msembo ambao unasemwa na watu wa upinzani wa ODM. Huwa wanasema ni sasa na kama si sasa, ni sasa hivi. Kwa sababu tuko na Mheshimiwa mmoja hapa, nafikiri tumeungana vizuri kwa hili.

Napenda watu wa mlengo ule mwingine kwa sababu tunafanya kazi pamoja. Bwana Spika, katika Bunge hili ningetaka ujue ya kwamba serikali na upinzani wanafanya kazi pamoja. Nimetazama na kuona upande wa upinzani wanaingia watu wawili ama mmoja lakini leo wako wawili hata kama Mheshimiwa Kamara ni wa upande wetu. Upande ule mwingine hawako wengi lakini najua wanatetea maslahi ya wananchi kwa sababu wako na huo mwito.

Nawapongeza sana watu wa upinzani na ninajua mtaniunga mkono ili tuweze kupitisha huu mswada. Wale ambao hawana maji ya kutosha na nafikiri wataendelea kupata, najua wataniunga mkono ili tukitoka hapa, tuhakikishe ya kwamba NAWASCO imepeleka maji huko. Kama watashindwa kupeleka na mifereji, wapeleke na lori kwa sababu tuko na magari ya kubebea maji ambayo itapeleka maji Doldol na wananchi waweze kusaidika.

Najua nikiangalia Mheshimiwa Leshuel, naona akicheka na kufurahi kwa sababu hapa tunataka kusaidia wananchi ambao tunawakilisha. Bwana Spika, ninaomba kwa unyenyekevu Mheshimiwa ambaye ndiye *Chief Whip* wa upinzani, Mheshimiwa Umija, aniunge mkono na kuafiki huu mswada. Asante, Mheshimiwa Spika.

*(Hon. Catherine Umija seconded)*

*(Question proposed)*

**Hon. Simon Kanyutu:** Thank you, Mr. Speaker. I stand to support this motion. Though the tariffs are high, the Hon. Members should first appreciate because they are getting water. There are areas where getting water is an issue. Mr. Speaker, they should not complain but what they should be complaining is the added charges when you delay in payment.

I am sure that water is a necessity and maybe the concerns which they are raising, some of us who come from remote areas spend more per day. For example, most of us from the rural areas, we offer the motorbike people to fetch water for us and a single Jerri can costs us Kshs.30. Per homestead, you must spend more than ten and so per day you spend almost Kshs.300. If you

calculate that, within 30 days that is almost Kshs.9, 000. I am sure that even as they complain of tariffs being high, none of them usually pay that amount.

Mr. Speaker, it is in order for tariffs to be down but they should also appreciate that water is sufficient. There are areas where even getting water is an issue. It is good that we do not oppress our people, it is also good that they get clean water because there is a cost. Let us also ensure that the cost is not exaggerated. We have a minimum cost that each and every person will be able to cater.

I am also sure that we have the economic status we are in in our country, getting a shilling in the pocket is an issue. Even the Hon. Member who is talking of the issue of bottom up is aware of what is really touching our people. They really require money in their pockets. Even paying for minimum tariffs is a challenge, because getting a coin in their pockets is also a challenge. There is no money circulation but let us hope that if we bring the tariffs down, it will be a benefit to our people and each and every person will be able to access clean water for their consumption. Thank you and I wholly support the motion.

**Hon. Paul Leshuel:** Thank you, Mr. Speaker. I also stand to support this motion. The motion is clear and I am so happy because it is giving a clear message that according to the constitution of Kenya, everybody has a right to clean water. The question which now lands in my mind is, when will Kenyans get clean water because that is the big issue? In some areas, we share water with elephants and domestic animals and this is in the constitution. So, when will that time come? This is a question and a responsibility of every leader to ensure that all Kenyans have got clean water.

Mr. Speaker, it is also clear in this motion that according to the Water Act, 2016, the board have got a mandate to review the tariff. So it is also clear that it is the responsibility of the board to make sure that every now and then they review the tariff. The issue here is the objective of this motion, to urge the County Government and the board concerned to review the tariffs so that they can favour everybody.

Mr. Speaker, when the Member here gives a directive that after this, this will happen, this is a motion but not a law and the motion is to give you an indicator that this must happen, based on the quotation or the Act which is there. So Mr. Speaker, I am very sure that the people concerned, immediately they get this motion they will be able to know what will follow next. I am also happy that the Members who are here understand other areas where people don't get water at all but we are here to help each other to ensure that after the tariffs are reviewed, we are also considering those areas to ensure that there is water.

We have got a challenge in this county. We have got some arid areas which need a very serious intervention in issues of water and other things. So, I support the motion which is very clear and according to the public demand, the concerned people should also revisit the tariffs which are there.

I am sure that it is not the board of that service provider who came in the morning and caused the tariff to come that amount, but the previous government decided on that. Now that this is a new government, we must go back to the law and ensure that everyone maintains the law. I need to tell the Members here that we are lucky because clean water is very important for

everybody. I am sure that within a very short time we will get this board to provide us with water in Doldol and other areas.

I am sure that we are going to come up with another motion here complaining that they are charging people from Chumvi a lot of money. So, this is very important for us to see whether the charges are within the law or they are just exaggerating. I want to appreciate and thank the Member who sat and thought about this motion because it is very important. It is very important to ensure that our people get clean water and in a very affordable way.

Mr. Speaker, we know that economically the country is not good and everybody is crying over scarcity of money. I am sure that we will continue because when you see the climate change, even the rain is not coming in a good way. So, I am expecting that even to April we will still be having problems in this Laikipia. Therefore, it is our responsibility as Members to ensure that every now and then, we think of our community and how they are going to survive and sustain themselves. We cannot sit here and allow other to people suffer and they have made us to be here. I am so happy and I want to thank the Member for this motion because I am sure that it is going to bring change in tariffs which we are complaining about.

**Hon. Benson Kuria:** Asante sana, Mheshimiwa Spika. Kabla niunge mkono mswada wa *Chief Whip*, mimi mwenyewe niliweza kuchagua Naibu wa Spika na naona sana anatamani kukaa sana kiti cha Kiongozi wa Walio Wengi. Sijui kwake ni wapi. Kabla niendeleo...

**Speaker:** Hon. Deputy Speaker, Standing Order requires you to sit on your seat. Thank you.

**Hon. Benson Kuria:** Asante, Mheshimiwa Spika. Nikiunga mkono mswada ambao tumeletewa na Mheshimiwa Gathoni. Ningependa kwanza kumuuliza *Chief Whip*, kwa sababu kuna faini ambayo imewekwa mahali pale ya shilingi elfu moja, ikiweza kuondolewa, sababu kuu ilikuwa ni nini? Ningependa kabla niendeleo na huu mdahalo *Chief Whip* aweze kunijibu.

**Hon. Stephen Ndiritu:** Asante, Bwana Spika. Nafikiria ya kwamba Mheshimiwa Benson anataka ufafanuzi zaidi sababu ya kuongezwa kwa hii elfu moja. Niweze kumuarifu ya kwamba ile sababu ilifanya waongeze hiyo elfu moja, walisema ya kwamba kama unafaa kulipa maji tarehe moja na kisha uchelewe kulipa hiyo siku, basi siku anayofuata wanaongeza elfu moja. Hata mishahara ambayo huwa tunalipwa hapa. Mimi najua ya kwamba sheria inasema niwe nikilipwa tarehe ishirini na nane lakini wakati mwingine, huchelewa na ninapata tarehe tano au sita.

Kwa hivyo, ndio hapo tunasema ya kwamba kuchelewa sio shida lakini shida ni vile wanaweka hiyo pesa nyingi. Hata kama ni faini, hauwezi ukapigwa faini zaidi ya zile pesa ambazo unafaa kulipa. Hata kama wangesema 5% au 1% au mia moja, ingekuwa afadhali lakini hii ni kama ukora na wizi. Hawa ni kama wezi wa kimabavu na hata wanafaa kuwa jela. Hivyo ndivyo ningetaka kumwelekeza.

**Speaker:** Hon. Benson, are you satisfied?

**Hon. Benson Kuria:** Bwana Spika, nimeridhika na huo ufafanuzi vile Mheshimiwa Ndiritu ameweza kunipa mwongozo. Ni vyema niseme katika hili Bunge kwa sababu ni Bunge la kutunga sheria ya kwamba wakati tunapoondoa kipengele cha kusimamia sheria, kuwe na mikakati dhabiti kabisa. Kama kuna sheria ambayo itaweza kuondolewa, kijulikane ya kwamba katika hili Bunge la tatu kuna sheria imetungwa ya maji kwa sababu ukiangalia NAWASAKU, iko upande

wa Laikipia Magharibi na Laikipia Mashariki. Ukiangalia upande wa Laikipia Kaskazini, hakuna mradi wowote a maji. Kwa hivyo ningependa itakapopitishwa kwamba ule mradi wa maji ambao tunafaa kupata, nasi katika Laikipia Kaskazini...

**Speaker:** Order Member! Hon. Theuri?

**Hon. Antony Theuri:** Mr. Speaker, I need a clarification from the Hon. Kamala. What is NAWASAKU because from what I understand, we only have NAWASCO and NYAHUWASCO? We are reading from two different scripts, He is either speaking of Kitui or any other county but not Laikipia.

**Speaker:** Hon. Member, just a clarification required.

**Hon. Benson Kuria:** Kulingana na ufafanuzi wangu, mimi najua ya kwamba NAWASAKU ni Nanyuki na NYAWASAKU ni Nyahururu.

**Hon. Antony Theuri:** Being the representative of the great people of Nanyuki, we do not have any entity named NAWASAKU. He is reading from a different script and I do not want to be sued by any entity. It is NAWASCO and not NAWASKI.

**Hon. Stephen Ndiritu:** Nilikuwa nataka kumpatia mwelekeo kwamba tunaongea kuhusu NAWASCO ambayo ni *Nanyuki Water and Sewerage Company*. Upande wa Nyahururu inaitwa NYAHUWASCO. Kamala hajakosea sana, ni 'U' tu anaweka. Kwa hivyo, atapindua hiyo U aweke 'O' iwe NAWASCO na NYAHUWASCO.

**Speaker:** Members, let us continue. Perhaps it is pronunciation of words.

**Hon. Benson Kuria:** Mheshimiwa Spika, yale tunaongelea ni kuhusu Kaunti ya Laikipia na mimi sio mtu wa Kitui, ningetaka Naibu Spika aniombe msamaha. Yale ambayo ninalenga sio ya Kitui lakini ni kuhusu Kaunti ya Laikipia ambapo tunasimamiwa na Gavana wetu, Joshua Wakahora Irungu na Spika wetu Lantano Nabaala. Wakati anaponiambia maneno ya Kitui, ananikosea na kwa hivyo, aniombe msamaha kwa sababu mimi niko *form* na pia *network* na ninajua mahali ninapoelekea. Naibu wa Spika anafaa kuniomba msamaha kwa sababu ametenda dhambi.

**Speaker:** Hon. Salim, the floor is yours before I make determination.

**Hon. Salim Edung:** Nashukuru sana. Kabla sijaingia katika mdahalo nataka kupongeza Wajumbe wa Bunge la Laikipia wakiongozwa na Spika na Naibu wa Spika, Karani wa Bunge na pia Gavana. Napatiana pongezi yangu kwa sababu ya ile tamasha ambayo tulikuwa nayo. Mlinishika mkono na nikaamini ya kwamba sisi wote ni mandugu. Kabla sijaanza kuchangia. Ningetaka kuambia Wajumbe wote katika hili Bunge ya kwamba muendeleo kwa huo moyo kwa sababu leo ni mimi na kesho ni mwingine. Lazima tuwe na huo moyo tukisaidia wananchi wa Laikipia.

Nikiingia katika mswada, haya mambo ya maji yanatusaidia sana kwa njia moja au nyingine kwa sababu hizi kampuni zinaongezea maji ya Nanyuki na pia Nyahururu. Sisi tukiwa katika Laikipia Kaskazini, hatuna mradi kama huo. Sisi tunatetea Laikipia nzima na sio sehemu moja ya Laikipia. Nikirejelea katika NAWASCO, ile ada ambayo wameweka pale, ile ni ada ya juu kwa sababu kuna mtu ambaye hatapata ile pesa.



Katika serikali ambayo tuko nayo inataka kuinua juu yule ambaye yuko chini. Tungeomba hiyo kampuni ya NAWASCO wajaribu na kuangalia hata kama sio hiyo tarehe moja ambayo wanaitisha ile pesa, ningepomba katika hili Bunge ya kwamba waweze kuangalia maslahi ya wananchi ambapo sisi tunasimamia.

Katika Laikipia, kuna watu ambao wana uwezo na wenye hawana na lazima iangaliwe kwa makini sana kwa sababu hiyo itakuwa njia moja ya kunyanyasa wale wasiojiweza. Katika sheria, lazima kila mmoja aangaliwe. Mimi naunga mkono mswada huu ulioletwa na Mheshimiwa Mary Gathoni kwa maana inaangalia maisha ya wananchi kwa sababu ukikosa maji, maisha yanakuwa magumu.

Tukiangalia sehemu za Laikipia Kaskazini, naunga Mheshimiwa Paul Leshuel mkono anaposema ya kwamba maji yenye tunakunywa pale sio maji safi. Kwani mifugo na wanyama kama ndovu na nyani wote wanakunywa maji hayo, kisha maji hiyo ndiyo yanayonyiwa na wanadamu na inaadhiri afya ya wananchi hao.

Sisi tungeomba tunapoendelea kuangalia mambo ya NAWASCO, nasi pia tuangalie Kaskazini mwa Laikipia ili wapate maji angalau hata ya *Bowser* ili wapate maji kama watu wengine. Kwa hivyo, mimi naunga mkono na ningependa pia kuwaeleza wenzangu waunge mkono kwa sababu inajali maslahi ya watu wetu. Asante, Bwana Spika.

**Speaker:** Thank you very much. Originally, I thought that you would stand to interject what is on the floor but because Hon. Benson Kuria had not finished his address to the House. Are you willing to proceed with your contribution?

**Hon. Benson Kuria:** Bwana Spika, naomba naibu wa Spika kwanza aniombe msamaha juu mimi sio wa Kitui, bali wa Laikipia. Nawakilisha walio wachache katika chama cha UDA na walinichagua nikiwa Laikipia, wala sio Kitui.

**Speaker:** Okay. I just want a clarification from Hon. Antony Theuri. Did you imply that Hon. Benson Kuria is from Kitui?

**Hon. Antony Theuri:** Asante, Bwana Spika. Niruhusu tu niongee Kiswahili kwa maana najifunza. Kwanza, ningependa kusema Mheshimiwa Benson Kuria anastahili aeleele ya kwamba sisi binadamu tuliumbwa ili tukae karibu na watu. Mimi kama mwanasiasa, napenda kukaa karibu na watu na ninapokaa na wazee, wananipa hekima ya miaka mingi.

**Hon Simon Kanyutu:** Mr. Speaker, is it in order for Hon. Deputy Speaker to claim that being a social person, you need to be closer to the people? There will come a time when maybe you the Speaker will sit before the mace. Is it in order please because being given a designation and a position, you ought to sit in that same position? There is no way you can lead the House seated in the Clerk's chair. Let him clarify why he needs to relocate from his position.

**Speaker:** Thank you, Mr. Kanyutu and Hon. Members. Our Standing Orders stipulate that everyone sits in the plenary in their official positions. I would like to put that to rest, that every person who holds a position, indicated and marked, is compelled to sit in their official sitting spaces. Thank you. The Hon. Antony Theuri, I would like you to respond in a brief manner and after this, I will give a determination.

**Hon. Antony Theuri:** Asante sana, Bwana Spika. Mimi sitaomba msamaha, msamaha yenye nitaomba ni kwa ajili ya kuketi kwa kiti chenyewe na hilo halitafanyika tena. Lakini kwa Mheshimiwa mwenzangu, sitamuomba msamaha kwa maana nilikuwa tu natoa kama mfano.

Yeye kama dereva wa hili gari letu ya kuchangia hii mswada, amelipeleka gari lenyewe vibaya na anafaa kuomba msamaha kwa kutuita NAWASCO. Kwa hivyo, anafaa kufanya utafiti wake vilivyo kabla ya kuchangia. Asante sana.

**Speaker:** Are you confirming to the House that you did not imply that the Hon. Member is from Kitui?

**Hon. Antony Theuri:** Mimi najua sana hatoki Kitui. Nilisema kwenye alisema ndio husemwa kule kitui. Mimi napenda watu wa Kitui na sina uhasama na wao.

**Hon Simon Kanyutu:** Mr. Speaker, I can defend the Deputy Speaker. The Moment the Hon. Member talked about NAWASCO, the Deputy Speaker thought he is using the accent from Kitui because that is how people from there talk. He did not imply that the Hon. Member is from Kitui. Thank you, Mr. Speaker.

**Speaker:** The Hon. Benson Kuria, are you satisfied with the explanation? Kindly do so in short so that we are able to proceed with our motion.

**Hon. Benson Kuria:** Mheshimiwa Spika, niko sawa na nimeridhika na Naibu Spika hata akiwa kijana mdogo, kwa maana ni kijana mchapa kazi.

**Speaker:** Thank you very much. Proceed with the motion.

**Hon. Benson Kuria:** Bwana Spika, Kaskazini mwa Laikipia ndiko pahali ya walio wachache na kunayo uhaba wa maji. Tunapongea kuhusu maji, Kaskazini mwa Laikipia inafaa kushughulikiwa kwa njia iliyo mwafaka kabisa. Naunga mkono huu mswada wa Mheshimiwa Mary Gathoni nikisema kwamba utaweza kubadilisha mikakati ya Laikipia mzima.

**Hon. Catherine Umija:** Asante sana, Bwana Spika. Nitajaribu kuongea kwa Kiswahili kwa mara ya kwanza na ikinipiga chenga, tafadhali msinikosoe sana. Hiyo sanasana namwelekezea Naibu Spika. Nataka kushukuru Mheshimiwa Mary Gathoni kwa kuleta mswada katika Bunge kuhusu ada ambayo inatozwa kwa maji. Kusema kweli, hiyo ada iko juu kwa maana shilingi elfu moja ni mingi sana kuwatoza ada wananchi baada ya siku kadhaa.

Kwa mfano, ukiwa na bili ya shilingi mia mbili na utozwe ada ya elfu moja, hiyo ni kama mara tano ya hiyo pesa. Mwezi huu, nimekosa kutoa hiyo pesa ya mia mbili kisha nitozwe ada ya shilingi elfu moja. Mwezi ujao bili yangu inakuwa shilingi elfu moja na mia mbili na nikikosa kulipa hiyo, bili ya mwezi ingine, bili yangu inafika shilingi elfu moja mia nne.

Mwananchi wa kawaida ambaye atashindwa kulipa shilingi mia mbili, atawezaje kulipa shilingi elfu sita baada ya miezi mbili ama tatu? Hiyo ni haki kweli? Ni haki kwa mwananchi kupata maji safi kulingana na sheria na kutozwa ada ya shilingi elfu sita? Mtu anayefaa kulipa bili ya shilingi mia mbili kutozwa ada ya shilingi elfu sita ni pesa mingi sana.

Watu wengi hasaa wa kutoka maeneo ya Nanyuki na Thingithu wanaopewa maji na NAWASCO, wamekatiwa maji kwa sababu hawawezi kulipa hiyo ada ikawabidi wanunue maji kwa shilingi ishirini ama thelathini kila siku na hiyo haifai.



Nataka kuunga mkono mswada huu nikisema kuwa tuweze kushukisha hiyo ada ikuwe angalau asilimia tano ya hiyo bili ya mia mbili yenye mwananchi wa kawaida anaweza kulipa. Naelewa kuwa NAWASCO wakitiza ada hiyo, ni njia moja ya kupata pesa za umma bali hawafai kuwatoza chenye wananchi hawataweza. Asante sana.

**Hon. Antony Theuri:** Asante sana, Bwana Spika. Nasimama kwa kuchangia ingawa leo nimechokozwa sana, bali nashukuru mungu kwa maana leo ni siku yangu ya maombi na nina amani tele moyoni na hivyo, nawasamehe wote.

Nikichangia katika huu mdahalo wa maji, naomba neema ya mungu kwa sababu naweza onekana kama mchochezi bali nitasema ukweli mtupu. Mheshimiwa Stephen Nderitu alivyosema, sisi watu wa Nanyuki na Thingithu tumekuwa tukiibiwa kwa mabavu kwa muda mrefu kwa mambo ya maji.

Mimi nimekuwa mtu wa jua kali kwa miaka mingi na kwa neema ya mungu, saa hii ninawakilisha watu wa Nanyuki na wamenitoa hiyo nguo ya kazi nilikuwa nimeivaa. Kwa hivyo, mambo ya maji naelewa kwa undani kabisa. Mimi ni kiwakilishi kizuri zaidi ya “*bottom Up*”

Utaeleza vipi Bwana Spika, ya kwamba sisi watu wa Nanyuki, Thingithu na Likii tulio wengi na tunatumia maji ya mia sita ama kidogo kuliko hizo, tunatozwa ada ya shilingi elfu moja. Hiyo, mimi naona ni wizi wa mabavu. Kwa mfano Bwana Spika, najua wewe ni tajiri kabisa na unatumia maji ya shilingi elfu ishirini na kwenda juu na sababu ya ile tabia ya matajiri kusahau kulipa maji, unapata amekaa miezi sita bila kulipa maji kisha wanapata wako na bili ya zaidi ya laki moja. Yeye mwenyewe akitozwa faini ya elfu moja, yule mama yangu mwenye yuko Likii akiwa na bili ya mia sita anaongezwa elfu moja juu.

Sasa mimi nauliza, haki iko wapi? Inaonekana sisi maskini wenye mungu anatutajirisha kwa maana hatutabaki hivyo, tunawatumikia matajiri. Inaonekana maskini ndio wamekuwa wakishikilia huu uchumi wa maji. Naunga mkono mia kwa mia watu wakitozwa ada ya maji kwa maana kampuni hiyo inahitaji pesa kukuwa, bali wasitumie kama binu ya kutugandamiza. Mimi ningetaka haki itendeke.

Kama Mheshimiwa Catherine Umija alivyosema kwa Kiswahili chake sanifu, kwa maana amekuwa akijificha na anaweza kuwa mwalimu mzuri kabisa, wakae chini na sisi tujadiliane kama vyenye tuliongea. Hii ni biashara na pia wakumbuke kwamba maji ni uhai na tunaweza kasirika siku moja na tuamue kuwanunulia wakaazi wote wa Laikipia matanki, na mungu atupee mvua kisha wafunge biashara yao. Wasitufanyie chenye *Kenya Power* wanavyotufanyia kwa kututumia stima wakati wanataka.

Waje tuketi chini na tukubaliane, watu watozwe ada ya asilimia kiasi gani kwa maana hiyo ndio inayostahili. Hakuna kampuni wasio na kiwango fulani ambacho hawafai kupitisha ada zao. Itakuwaje NAWASCO wamekuwa na ubinafsi hadi wanakaa chini wakila samosa na maandazi na kuamua kupandisha ada watakavyo?

Kabla niketi Bwana Spika, isisahaulike kwamba sio watu wote wanapata maji hayo. Kuna pahali mtu aliekewa maji miaka tano iliyopita na wakati huu hawapati maji hayo na bado wanalipa ada. Kama sio wizi wa mabavu, basi ni wa bunduki.

Mimi ningesema na ningetaka ikue changamoto kwa Mheshimiwa Paul Leshuel mwenye tulimpea jukumu ya Kamati ya Utendajikazi, isikue kazi yetu ni kuja kupiga kelele hapa kisha

inasahaulika hapa. Yale tumeyapitisha hapa Bwana Spika na nikiwa Mwenyekiti wa Uhusiano, nitamfikia Mheshimiwa Paul Leshuel ili yote tunayofanya hapa ipitishwe.

Kabla turudi kutoka likizo kama tutapitisha huu mjadala, mambo ya maji inafaa kuwa imeshughulikiwa na hiyo ada ya shilingi elfu moja itolewe. Pia Bwana Spika, mimi ni shahidi kwamba Gavana wetu amekua mkuu wa maji na tulisimama naye mahali fulani. Kama biblia inavyosema, neno la mfalme ni sheria. Akatamka nikiwa hapo na akasema hiyo shilingi elfu moja itolewe na bado ipo hadi wa sasa. Inavyoonekana, hawa watu hawamheshimu Gavana wetu.

Mjadala ya kwanza tukirudi kutoka likizo kama utatupa ruhusa Bwana Spika, Mheshimiwa Paul Leshuel aje aseme hiyo ada imetolewa kwa sababu hawa watu wametuzoea. Kila uchao unapokea simu ya kwamba maji imeongezeka bei, kesho unaambiwa jambo lingine. Ningeomba jumba hili tukufu lipewe heshima, kama tutasema hiyo elfu moja itolewe, basi itolewe. Hiyo sio ofisi ya mtumwa, inastahili heshima yake na kama watu hawatafanya kazi inayostahili, tutawatoa hata kama ni ndugu ya mmoja wetu hapa.

Hatutakubali kuchapwa na wananchi kwa sababu ya vitu inayoheshimika. Mimi naomba Bwana Spika na naomba jumba hili hiyo ada ya elfu moja itolewe na ada yenye wananchi wanaweza kumudu, iwekwe ndio watu wapate maji kwa wingi. Tuisahau kwamba tutawamulika zaidi kwani kuna pesa ambazo zinasemekana ni za michezo zenye ziko huko. Tutafika hapo na mambo ingine mengi

Hiyo nyumba ya *NAWASCO* ambayo nitaita nyumba kwa sasa, tutaiangalia kwa macho mawili. Nitaiangalia vizuri sana nihakikishe ya kwamba haki imetendeka. Nikumbushe Mjumbe Paul Leshuel, sasa kazi yako itaanza kuonekana zaidi. Mimi nitakufuata, jambo ambalo linapitishwa hapa unahakikisha umeleta ripoti hapa. Asante sana, Bwana Spika.

**Speaker:** Thank you, Hon. Theuri. The floor is still open. Thank you very much. Without much ado, I will now invite the mover to reply.

**Hon. Stephen Nderitu:** Asante sana, Mheshimiwa Spika. Nafikiri mwanzo kabla nifanye majumuisho yangu, ningetaka kupeana ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Theuri kwamba kama ndugu yangu anafanya kazi kule *NAWASCO*. Alikuwa anatoa mfano, isieleweke vibaya Wajumbe wafikirie ndugu yangu anafanya kazi huko.

Ieleweke hakuna ndugu yangu anafanya kazi kule, labda iwe kuna mtu wa familia huenda *NAWASCO*, ni kufanya malipo kule ya ada ya maji. Kwanza, mimi nataka kushukuru kwa vile Wajumbe wameweza kuchangia huu Mswada, na wakachukua kwa njia ambayo inafaa. Kama kuna nyakati zingine Mheshimiwa Leshuel ananinogonozea ya kwamba tunazungumzia mambo ya ada, hatuzungumzi mambo ya ada za maji lakini nikamfahamisha atakapokuwa akienda kuangalia hiyo mambo, ataipata pale.

Mwanzo pia nimshukuru Mjumbe Kanyutu, kwa vile amesema ya kwamba watu wa Nanyuki na Nyahururu wanalalamika juu ya maji. Nimweleze ya kwamba tunalalamika kwa sababu tuko nayo. Kama huna kitu, huwezi lalamika kuna shida na ndiyo maana unapata Mjumbe Leshuel, halalamiki sana kwamba wao wanalipisha ada kubwa.

Mimi nafikiria ya kwamba ni kama mfano wa mtoto ambaye amezoea kunyonya na mzazi anapokosa kumnyonyesha, lazima huyo mtoto atalalamika ya kwamba hajapata maziwa. Ndiyo

maana tunalalamika ya kwamba wananchi wetu wanaumia na pia ndio wako na shida ya kuongezewa bei ya maji na pia kutozwa ile faini kubwa.

Ningetaka kusema ya kwamba, wale ambao wametoka upande wa Laikipia Kaskazini kama Mjumbe Leshuel na Mjumbe Benson Kuria, ambaye anawakilisha walio wachache Laikipia, pia nimshukuru kwa sababu anatetea walio wachache vilivyo. Uendeleo kwa huo moyo. Naelewa Chama inakuangalia na macho mawili na sisi ni shahidi ya kwamba unatetea walio wachache kwa njia ifaayo.

Niweze kusema ya kwamba kila mtu yuko na haki ya kupata maji. Tutasukuma serikali tukiwa wote tuhakikishe ya kwamba pia wale wako kule Laikipia Kaskazini ambapo Mjumbe Leshuel, Lempaira na pia Salim anawakilisha, pia tuhakikishe ya kwamba wamepata maji safi ya kutumia.

Nimehuzunika kupata taarifa mahali ambapo Mjumbe Leshuel anawakilisha, anapata Maji ndovu pia wanakunywa yale maji. Ndovu ni mnyama mkubwa na anachafua yale maji, kwa hivyo ninasikia huzuni kwa sababu wale wako kule ni wananchi na pia wangehitaji kupata maji safi. Ndiyo maana ninaomba Serikali ya Laikipia itumie yale magari tuko nayo ya maji, kusafirisha maji katika sehemu hiyo kwa wale wataweza kupatikana kwa haraka.

Niweze pia kuweka mambo wazi ya kwamba, kampuni ya *NAWASCO* na *NYAHUWASCO* sio kampuni ya kutengeneza faida. Hiyo ieleweke hivyo na hakuna pahali sheria inaruhusu watengeneze faida. Kama kuna siku wataripoti wametengeneza faida, hiyo ni kinyume na sheria. Wanafaa kutafuta pesa ya kulipa wafanyikazi na kuweka vituo za maji.

Siku moja tutapata wamepata faida zaidi hata kama ni ya elfu moja, siku hiyo wataenda jela kwa sababu hiyo inamaanisha wanafanya kazi kinyume na sheria. Sisi ni watu tunapenda kufuata sheria, mimi ningeomba wasitengeneze faida. Wahakikishe ada ya maji imerudi chini ndiyo mwananchi aweze kupata maji kwa njia rahisi na pia kwa bei nafuu.

Kwa hayo machache, nataka kuwashukuru Wajumbe wote kwa kuchangia huu Mswada, na ni mswada utasaidia watu wa Laikipia na pia ni wa maana sana, kwa wakati huu kwa sababu inajulikana maji ni uhai. Watu wakikosa maji huenda uhai wao ukakatizwa. Kwa hayo, naomba sisi wote, tuungane pamoja na tuunge huu mswada na pia tupitishe kwa kauli moja ili tuweze kupeleka kwa Kamati ya Utekelezaji na wale ambao tuko karibu na hizi kampuni tuweze kufuatilia na kuwaokoa wananchi ambao wanateseka kwa kusukumwa na hii kampuni.

Asante sana, Bwana Spika. Nakuheshimu na kukuvulia kofia kwa sababu unatupeleka vizuri. Mimi naona wewe unatosha na mambo yako iko sawa. Kwa hayo, mungu akubariki na akutende mema.

*(Question put and agreed to)*

## ADJOURNMENT

**Speaker:** The sittings of this House now stands adjourned until tomorrow Thursday, 8<sup>th</sup> December, 2022 at 2.30 p.m.

The House rose at 3.28 p.m.